Aprili 16, 2015

FBME Limited: Muhtasari wa mkutano wa FinCEN na Hogan Lovells

Tarehe 9 Aprili, 2015, FinCEN, idara ya Hazina ya Marekani ilichapisha makala mabayo ilitoa kwa muhtasari wa mkutano wake na wanasheria wa FBME Benk, Hogan Lovells. Taarifa ilitolewa na muhtasari mfupi sana kuhusu mkutano huo. FinCEN haikutoa maoni yeyote wala taarifa mahsusi.

Taarifa ya FinCEN inapatikana kwenye tovuti http://www.regulations.gov/! yenye;D=FINCEN-2014-0007-0006 na hiyo ripoti inasomeka hivi:

"On January 21, 2015, representatives of FinCEN met with counsel for FBME at FinCEN's offices to discuss written comments that FBME had previously submitted regarding FinCEN's Notice of Proposed Rulemaking (NPRM), dated July 15, 2014, and Finding, dated July 15, 2014, which identified FBME as a primary money laundering concern under Section 311 of the USA PATRIOT Act. Representing FinCEN were Stephanie Brooker, Richard May, Lawrence Scheinert, Ryan Williams, Carlton Greene, and Mona Sahaf. Representing FBME were attorneys Jeanne Archibald, Ethan Kate, Beth Peter, Evans Rice, and Peter Spivack of Hogan Lovells, LLP. FBME provided information concerning the applicability of the statutory factors set forth at Section 311 of the USA PATRIOT Act to FBME; the factual basis of the Finding; the sufficiency of FBME's anti-money laundering (AML) compliance program, including changes that FBME has made to its AML program; and the relative impact of the NPRM."

***

FBME imefurahia makala hiyo kwa sababu inaleta mwanga kuwa kuna ushirikiano baina ya Benki na wanasheria kwa upande mmoja na FinCEN kwa upande wa pili. FBME inatarajia kuwa hii itaonyesha njia ya kufikia muafaka na mwisho wa Ilani na vikwazo dhidi ya benki.

Mkutano wa tarehe 21 Januari 2015 baina ya Hogen Lovells na FinCEN ulikuwa wa mafanikio. Katika mkutano huo, Hogan Levells wali ainisha na kuelezea kuhusu maelezo yakini waliopeleka FinCEN kufuatia utolewaji wa Ilani ya maamuzi (NPRM) na ilani ya uchunguzi(NOF).

Ibara namba 311 Sheria ya Wazalendo ya Marekani inaelezea kuwa kuna hatua muhimu za kufuata kabla FinCEN haijatoa uamuzi. Hizo hatua ni:- Kwanza, kutafakari kama hatua hizo zimechukuliwa na mataifa mengine au taasisi kubwa; pili, kuchambua kwamba je huu uamuzi wa tano wa ilani utaleta athari za hasara ya kiushindani na gharama zisizo za kilazima kwa mashirika yanayo shughulika au yaliosajiliwa Marekani; na tatu, kuangalia je uamuzi huu ungeleta muamko hasi kiasi gani kwa biashara halali zinazohusu FBME.

Katika mkutano huo na FinCEN, wawakilishi wa FBME waliwaelezea kuwa kutokana na mambo ya kisheria, kuna kila sababu hiyo ilani, NPRM, inahitaji kuzuiwa. Kuhusiana na sababu zilizotajwa hapo juu, wanasheria wa FBME waliwaeleza kuwa hakuna nchi wala taasisi yeyote ikiwemo Umoja wa Ulaya EU, Benki Kuu ya Tanzania BOT wala Benki Kuu ya Cyprus CBC iliowahi kuitaja FBME kama chombo

kinachohusika katika utakatishaji wa fedha haramu. Wawakilishi hao wa FBME waliwaeleza kuwa endapo hatua hiyo namba tano itachukuliwa, ingeleta gharama kwa kampuni za Marekani, kwa sababu hiyo, haifai hiyo hatua namba tano ichukuliwe katika muswada wa mapendekezo.

Endapo hatua hiyo itachukuliwa ni wazi kuwa ingeleta maafa makubwa kwa wateja halali kwa maelfu wasiohusika na shutuma zilizotolewa na FinCEN. Hata hivyo, ilani pamoja na amri ya tano yalisha anza kuonyesha athari kwa wateja wa FBME. Ilani ya hatua NPRM na ilani ya uchunguzi NOF haikuweka wazi athari ambayo FBME benki ingepata wala kwa wateja wake, ingawa imeonekana wazi kuwa na madhara makubwa.

Kwa hali hiyo inaonyesha wazi kuwa hoja ya FBME ni muhimu, hatua ya NPRM yahitaji isichukuliwe.

FinCEN imesema kwamba FBME ilitoa taarifa zake kutokana na “hali halisi ya uchunguzi”. Haina shaka kuwa FBME imetoa nakala ya kurasa 700 ya hali halisi inayohusu uchunguzi uliofanywa kuhusiana na hilo, kuzuia utakatishaji wa fedha haramu, jinsi inavyo jitahidi kuongeza ufanisi kwa jambo hilo, na vilevile imeonyesha kuwa kuna kasoro ama taarifa isiyo sahihi kwenye ilani ya Marekani NOF. Wawakilishi wa FBME walitumia vigezo hivyo na vielelezo vya jinsi mipango ya kufuata taratibu ilivyoboreshwa, hatua hizo za sheria katika ibara ya 311 Sheria ya Wazalendo ya Marekani, na athari kwa nchi za Marekani, Cyprus na Tanzania endapo ilani ya NPRM itachukuliwa, zinaonyesha wazi kuwa hii ilani isichukuliwe.

Hogan Lovells, kwa niaba ya FBME inaendelea kuwasiliana na FinCEN ili hatua hiyo ya ilani ya NPRM isichukuliwe. Katika mkutano huo na mazungumzo mengine yalioendelea, FinCEN imetamka kuwa bado haijafikia uamuzi wa kuchukua katika ilani wa mapendekezo ya amri ya ilani.

FBME imekuwa ikisema mara kwa mara kuwa iko tayari kushirikiana na FinCEN katika kutokomeza biashara haramu kutoka kwenye mkondo wa taasisi na imesisitiza kuwa iko tayari kushirikiana na FinCEN bega kwa bega katika kufanikisha malengo hayo.

FBME, kwa upande wake inaahidi kuendelea kuwasiliana na FInCEN kupitia wanasheria wake. FBME inachukua fursa hii kutoa ahadi yake kuwa itawapa ushirikiano kamilifu FinCEN.

FBME itaendelea kuchapisha makala mpya kwenye tovuti yake , www.fbmeltd.com, mara tu watakapopata taarifa.